Toleo la Pili - **Mei , 2025**

**WIZARA YA AFYA**

**HOSPITALI YA BENJAMIN MKAPA**





# TOLEO MAALUMU

## MWAKA MMOJA WA WAZIRI WA AFYA NA MKURUGENZI MTENDAJI WA BMH

**#Kazi Iendelee.**










# Yaliyomo



JK aridhishwa na Huduma za Kibingwa zinazotolewa na BMH uk4


BMH yapokea mashuka yenye thamani ya Sh. Mil. 20 kutoka NMB uk5


BMH na Aga Khan waingia makubaliano kupambana na saratani uk.6


Prof. Makubi ateta na Menejimenti ya BMH kuleta matokeo uk.7


Shirika la LFTW kuongeza udhamini kwa miaka 5 BMH uk.8


Mhagama azindua huduma saba BMH, zitaongeza ufanisi uk.10


BMH ni ya kisasa, inayojali wagonjwa uk11


BMH washirikiana na Madaktari Bingwa kutoka Uholanzi uk.14


BMH, UDOM, Japan kujenga Kituo cha Umahiri cha Upandikizaji Figo... uk.16


Ujumbe kutoka Somalia wapata uzoefu wa mnyororo wa dawa... uk.19


Menejimenti BMH yapigwa msasa masuala ya Uongozi, Usimamizi uk.26


Mabalozi wakagua ubora wa huduma zitolewazo BMH uk.39



# Kalamu ya Mkurugenzi Mtendaji

**Ndugu msomaji,**

Karibu katika toleo hili maalumu la BMH Habari ambalo linaangazia mwaka mmoja wa mapinduzi ya huduma bora zilizo tolewa kuanzia juni, 2024 mpaka Juni, 2025.

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uhai katika kipindi cha mwaka huu mmoja pili namshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunipa nafasi ya kuiongoza Hospitali hii ya Rufaa ya Kanda ya Kati, kwani nami nimetimiza mwaka mmoja tangu kupewa nafasi hii.

Katika mwaka huu ndipo tumeweka alama ya kufikisha mgonjwa wa 50 kumpandikiza figo tangu kuanzishwa kwa huduma hii mwaka 2018, hii ni alama kubwa inayo ungana na malengo ya kuanzishwa kwa Hospitali hii kuwa ya umahiri katika matibabu ya figo. Aidha katika matibabu ya figo tumeanza kunavuna figo kwa upasuaji wa matundu madogo. Faida ya upasuaji huu, mtu aliyechangia figo anapona haraka.

Eneo lingine ni Huduma ya matibabu ya selimundu, tunayoifanya kwa kupandikiza uloto, inaendelea vizuri hapa Hospitalini. Sasa tumefikisha watoto 21 kuwapandikiza uloto toka Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipoizundua huduma hii Mei 13, 2023. Tumechaguliwa kuwa Kituo cha Umahiri cha upandikizaji uloto kwa nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Nawapongeza watumishi wenzangu kwa majitoleo katika kuwahudumia wananchi. Mwaka huu, tumechukua nafasi ya kwanza kwa kutoa huduma bora katika kundi la Hospitali za Rufaa za Kanda katika ushindi huu inatuongezea ari ya kuwajibika na kuendelea kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

Kipekee niwashukuru wananchi Kwa kuendelea kutuamini.

**Prof. Abel N. Makubi**
**Mkurugenzi Mtendaji**

# JK aridhishwa na Huduma za Kibingwa za matibabu zinazotolewa na BMH



**Rais** Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ameridhishwa na hatua za utekelezaji wa maono aliyokuwa nayo wakati akianzisha Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) ya kuifanya kuwa kituo cha umahiri cha matibabu ya figo, pamoja na huduma zingine za ubingwa wa juu.

Rais mstaafu, Kikwete, ameyasema hayo alipotembelea BMH, huku akibainisha kuwa kipindi cha nyuma watanzania walikuwa wanapata shida ya huduma za matibabu ya figo ikiwemo huduma ya uchujaji wa damu na hivyo kulazimika kuzifuata Nchi za jirani.

"Maono yangu wakati tunaanzisha BMH yalikuwa kuanzisha Hospitali ambayo itakuwa kituo cha umahiri nchini katika matibabu ya figo na huduma nyingine za ubingwa wa juu. Nimefurahi ndoto yangu imetimia na sasa BMH inatoa huduma za kibingwa za matibabu ya figo ikiwemo uchujaji wa damu, upandikizaji figo, lakini pamoja na hatua hiyo kubwa ambayo imefikiwa, haizuii BMH kuwekeza katika utoaji huduma za matibabu ya magonjwa mengine," amesema Dkt. Kikwete

Dkt. Kikwete ametembelea huduma mbalimbali za BMH ikiwemo upandikizaji uloto, huduma ya matibabu ya figo, matibabu ya moyo na jengo linalojengwa la matibabu ya saratani.

Dkt. Kikwete pia amefurahishwa na Serikali kuendeleza huduma za tiba ya figo na kupanua zingine ndani ya Hospitali ya Benjamin Mkapa.

"Hii ni Hospitali ya nyota tano, pamoja na kwamba tulipanga iwe kituo cha umahiri cha matibabu ya figo lakini tulitaka itoe matibabu mengine ya ubingwa wa juu na imesadifu hayo maono," amesema Dkt. Kikwete.

Dkt. Kikwete amefarijika kuona huduma za hali juu katika uchunguzi na tiba ya Moyo, pamoja na Upandikizaji Uloto.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Prof. Abel Makubi, amesema mpaka sasa BMH imefikisha watu 50 waliopandikizwa figo toka huduma ilipoanza.

"Tumeokoa bilioni 1.6 ambazo zingetumika kuwapa rufaa watanzania nje ya nchi kwa ajili ya upandikizaji wa figo," amesema Prof. Makubi




# Hospitali ya Benjamin Mkapa yapokea mashuka 1,000 yenye thamani ya Sh. Mil. 20 kutoka NMB

**Hospitali** ya Benjamin Mkapa (BMH) imepokea mashuka 1000 yenye thamani ya mil. 20 kutoka Benki ya NMB ya jijini Dodoma.

Akikabidhi mashuka hayo, Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Bi. Janeth Shango amesema kwa kutambua juhudi kubwa ya Serikali katika kuboresha huduma za afya nchini, hivyo tunaunga mkono juhudi hizo za maendeleo kwa kutoa mashuka ili kuweza kusaidia jamii yetu.

"Mashuka haya 1000 tunayoyatoa kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa yana thamani ya shilingi milion 20, hii ni katika ushiriki wetu katika jamii katika uwajibikaji katika kusaidia sekta ya afya, amesema Bi. Janeth.

Ameongeza kuwa Benki ya NMB inaushirikiano mzuri na Hospitali ya Benjamin Mkapa na kuomba kuzidi kuboresha mahusiano ili kuweza kuboresha huduma za afya.

Akipokea mashuka hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa Prof. Abel Makubi, ameishukuru Benki ya NMB kwa kutoa mashuka hayo na kuongeza kuwa mashuka hayo yatatumika katika kuhudumia wagonjwa hospitalini hapo.

"Tunaishukuru Benki ya NMB kwa msaada wa mashuka kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa wetu, mashuka haya yatasaidia kuwahudumia wagonjwa katika ubora zaidi," amesema Prof. Makubi.

Prof. Makubi ameongeza kuwa kwa sasa Hospitali ya Benjamin Mkapa ipo katika mchakato wa kuwa hospitali ya Taifa hivyo uhitaji wa mashuka ni mkubwa kwani tutahudumia wagonjwa wengi zaidi katika ukanda wa kati , kwa msaada wa mashuka haya Hospitali itapata ahueni kubwa ya kuweza kuwahudumia wagonjwa katika ubora zaidi.

Hospitali ya Benjamin Mkapa itaendelea kudumisha ushirikiano na mahusiano mazuri na Benki ya NMB katika kuboresha huduma za afya na kuboresha huduma bora zaidi kwa jamii ya kanda ya kati na mikoa jirani.

# BMH na Aga Khan waingia makubaliano kupambana na saratani




**Hospitali** ya Benjamin Mkapa kwa kushirikiana na Hospitali ya Aga Khan wamesaini Hati ya Mashirikiano katika utekelezaji wa Mradi wa Udhibiti wa Kansa Afrika Mashariki (East Africa Comprehensive Cancer Project - EA - CCP ).

Lengo la mradi huu ni kuhakikisha saratani inatambuliwa katika hatua za awali zaidi, kuboresha huduma za matibabu kwa kutoa huduma zenye ubora za matibabu ya saratani, kuwajengea uwezo na kubadilishana uzoefu kwa wataalam, kuimarisha uwelewa kwa jamii kuhusu umuhimu wa kufanya uchunguzi wa mapema wa saratani na kuboresha vifaa na miundombinu ya uchunguzi wa matibabu ya saratani katika hospitali zetu.

# Prof. Makubi ateta na Menejimenti ya BMH akisisitiza huduma bora na uwajibikaji wa matokeo



**Mkurugenzi** Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH), Prof. Abel Makubi, alikutana na Me¬nejimenti ya Hospitali siku moja baada ya kuripoti ofisini.

Prof. Makubi alikutana na Menejimenti kwa mara ya kwanza tokea alipo¬teuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa kwaajili ya na kutoa muelekeo wa Hospitali katika uongozi wake.

"Leo tumekutana ili tutambuane na nijue nina nguvu kubwa kiasi gani nitakayo saidiana nayo kufanya kazi na kuipeleka BMH kuwa Hospitali ya Kitaifa na ya kisasa katika huduma bora," amesema Prof. Makubi.

Akiongea na Menejimenti amewataka kuwasimamia wanaowaongoza kuhakikisha wanafanyakazi kwa kujituma, weledi, maadili na nidhamu ya hali ya juu katika kuwahudumia wagonjwa.

"Nafahamu mnafanya kazi nzuri inay¬oleta matokeo chanya BMH lakini wapo baadhi ya wataalamu wachache ha¬wafanyi vizuri kwa kuchelewa kazini na kuwahi kutoka ninawaonya hiyo tabia waambieni waache, lengo letu liwe moja tu kumuhudumia mgonjwa kwa viwan¬go vizuri, bila kuchelewesha na kuonge¬za ubunifu katika kutatua kero huku kila mmoja akiwa na moyo wa kuithami¬ni BMH kama nyumba yake (sense of ownership)," amesema Prof. Makubi.

Aidha, amesisitiza kutatua kero zote zinazowakabili wagonjwa ili mgonjwa anapoingia na kutoka Hospitalini asi¬toke na manung'uniko ambayo si ya lazima na yako chini ya uwezo wetu.

"Sitegemei kusikia malalamiko mengi kutoka kwa wagonjwa haswa yale yaliyo ndani ya uwezo wetu, kila mtu ajipange namna bora ya kuwahudumia wagon¬jwa kwa kasi na kuzingatia miongozo (SOPs)," amesema Prof. Makubi.

Prof. Makubi ameiomba Menejimenti ya BMH kumpa ushirikiano, umoja na kuwa na moyo, kushaurina, kushirikis¬hana na watumishi wote katika kutatua changamoto na kujishusha kwa wagon¬jwa ndugu na Watumishi wote hasa wa chini ambao tunapaswa kuwasilikiza na kuwasaidia .

# Shirika la LFTW kuongeza udhamini kwa miaka 5 BMH

**Shirika** lisilo la Kiserikali la Light for the World (LFTW) litaongeza udhamini kwa Kliniki ya Macho ya Hos¬pitali ya Benjamin Mkapa (BMH) kwa muda miaka mitano zaidi ili kuimarisha huduma ya matibabu ya macho BMH.

Mkurugenzi Mkazi wa LFTW, Ndg. Jo¬seph Banzi, amesema lengo la kuonge¬za mradi huo ni kuimarisha huduma ya macho katika Kliniki ya Macho ya BMH.

“Programu itahusisha kuwapatia vifaa tiba vya upasuaji, mafunzo kwa wa-hudumu, huduma mkoba (outreach) na huduma ya macho kwa watoto,” amesema Ndg. Banzi alipomtembelea ofisini kwake Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Prof Abel Makubi.

Ndg. Banzi amesema LFTW inad¬hamini Hospitali tatu nchini katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma ambayo ni Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH).

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH), Prof Abel Makubi, amelishukuru Shirika la LFTW kwa ushirikiano mkubwa na Kliniki ya Macho ya BMH.

“Nimependezwa sana na ushirikiano niliokuta na Kliniki yetu ya Macho na mafanikio yaliyopatikana,” amesema Mkurugenzi Mtendaji wa BMH.

Prof Makubi amewahakikishia LFTW kuimarika kwa kwa ushirikiano kati ya Kliniki ya Macho ya BMH na shirika hilo na kwamba ushirikiano huo utasaidia kusogeza huduma ya macho kwa jamii kupitia huduma mkoba (outreach).



# Christian Blind Mission kushirikiana na BMH kuboresha huduma ya usikivu na macho

**Shirika** lisilo la Kiserikali la Christian Blind Mission (CBM) litashirikiana na Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) katika kuboresha vifaa tiba na kuona namna bora ya kuboresha huduma za matibabu ya masikio na ma¬cho BMH.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la CBM Tanzania, Bi. Nesia Mahenge, amesema lengo la kutembelea hospitali ya Benja¬min Mkapa ni kuona uhitaji uliopo ka¬tika kuboresha huduma za usikivu na macho.



"Tumekuja kuangalia uhitaji wa Hos¬pitali katika kuhudumia Kanda ya Kati na mikoa ya jirani ya Dodoma" amese¬ma Bi. Nesia.

Ameongeza kuwa BMH wanampango wa kuipandisha hadhi kuwa Hospitali pili ya Taifa, kuboresha huduma za afya ya macho, usikivu na tiba itakayosaidia kurudisha katika hali ya kawaida viun¬go vilivyojeruhiwa na kuwa Kituo cha Afya cha Kitaifa kwa makundi maalum kwenye maeneo ya huduma za macho na usikivu.

Kwa upande wake Mshauri wa Kimataifa kutoka CBM, Dkt. Diego Santana amemshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa BMH Prof. Abel Maku¬bi kwa ushirikiano walioupata katika kushirikiana kuboresha huduma ya afya.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Prof. Makubi ameli¬shukuru Shirika la CBM kwa ushirikiano mkubwa walioutoa katika kuboresha vi¬faa na huduma za matibabu ya macho na usikivu.

"Lengo hasa la kututembelea ni kuo¬na maeneo ambayo tutashirikiana kufa¬nya kazi kwa pamoja katika masuala ya mafunzo na vifaa kwa wataalam wetu katika huduma za kibingwa na kibingwa bobezi kwa ajili ya kuboresha huduma ya usikivu na macho," amesema Mkuru¬genzi Mtendaji wa BMH.

Prof. Makubi amewashukuru sana CBM kwa ushirikiano na mchango wao kwa Hospitali ya Benjamin Mkapa kati¬ka kuboresha na kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora ya usikivu na macho.





# Waziri Mhagama azindua huduma saba BMH, zitaongeza ufanisi wa kuhudumia wagonjwa



**Waziri** wa Afya Mhe. Jenista Mhag¬ama amezindua huduma saba ka¬tika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) hivyo kuendelea kuimarisha huduma za afya nchini.

Akiongea wakati wa uzinduzi wa hudu¬ma hizo, Bi. Jenista amepongeza watumi¬shi wa Hospitali kwa ubora wa huduma ya afya.

"Nimpongeze Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali, Prof. Abel Makubi, na timu nzi¬ma ya watumishi wenzake kwa huduma nzuri na ufanisi katika kuboresha hudu¬ma," amesema Waziri wa Afya wakati wa uzinduzi wa huduma hizo.

Katika uzinduzi huo, Waziri Mhagama, amezindua maabara maalumu (skills lab) ambayo itawajengea ujuzi wahudumu wa Afya Kanda ya Kati na mikoa ya jirani.

Waziri Mhagama pia amezindua, vyum¬ba maalumu vya upasuaji vinavyotem¬bea (mobile theatre truck) kuwawezesha wataalamu kufanya upasuaji hata mbali na BMH.

Huduma ya tatu iliyozinduliwa na Mhe. Jenista Mhagama ni pamoja na kituo cha huduma kwa mteja (Call Centre) kwa BMH ili kurahisisha mawasiliano kati ya BMH na wateja wake.

Huduma nyingine aliyozindua ni vyum¬ba vipya vya upasuaji vitatu hivyo kufiki¬sha vyumba 11 na hivyo kuongeza wigo wa huduma ya upasuaji kwa BMH.

Waziri Mhagama pia amezindua Mion¬gozo ya Matibabu (SOPs), Huduma kwa Wateja wa BMH, Miongozo ya Idara ya Kutoa Huduma, Kujiendesha na Kujenga uendelevu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali, Prof Abel Makubi, amesema watumishi wa Hospitali wameshirikishwa kikamilifu ka¬tika kuandaa Standard Operating Proce-dures (SOPs).

"Niwasifu sana watumishi wangu wa BMH wameshiriki kikamilifu katika kuan¬daa SOPs ambazo zitatuongoza katika kutoa huduma," amesema Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali.

Akitoa neno la shukrani, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa BMH, Dkt. Deoda¬tus Mtasiwa, amesema kuanzishwa kwa Hospitali ya Benjamin Mkapa ni kutokana na tathmini za Hospitali kama saba za In¬dia, hivyo ndiyo tukaja na BMH.

"Hata mchoraji wa Hospitali hii ni mtan¬zania baada ya kufanya tathmini ya Hos-pitali kama saba za India ndiyo tukaja na BMH," amesema Dkt Mtasiwa.

# BMH ni ya kisasa, inayojali wagonjwa

**Waziri** Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tan¬zania, Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), amesema Hospitali ya Benjamin Mkapa ni Hospitali ya¬kisasa na inayojali wagonjwa kwa kiwango cha juu.

Mhe. Majaliwa aliyasema hayo alipotembelea banda la Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) kati¬ka kilele cha wiki ya utumishi wa Umma jijini Dodoma.

"Nawapongeza kwa huduma mnazozitoa ni za kisasa na zin¬azingatia utu, hatujasikia un¬yanyasaji wala vitendo vya rush¬wa kwa kweli tunawapongeza sana endeleeni kufanya kazi" alisema Mhe. Majaliwa

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu wa BMH, Bi. Prisca Lwangili akim¬karibisha Waziri Mkuu ameeleza namna BMH ilivyo toa Huduma na Kutoa elimu kwa wananchi kupitia maonesho ya wiki ya utumishi wa Umma.

"Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunayofuraha kwa kututembelea katika banda letu pamoja na huduma zinazotolewa hapa na BMH tumeendelea ku toa elimu juu ya huduma ambazo Serikali imewekeza kwa kiwango kikubwa ikiwa ni pamoja na matibabu ya Selimundu, matibabu ya figo ambayo tunapandikiza figo, matibabu ya moyo, saratani, aidha tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa Serikali chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanza nia kwa kutoa fedha za kuanzisha jengo la matibabu ya saratani na huduma za upandikizaji uloto am bazo ni za kitaifa na kimataifa," amesema Bi. Lwangili

BMH imekuwa ikitumia maonesho kama sehemu ya kusogeza huduma zake kwa jamii na kuzi tambulisha kwa Watanzania.



# Waziri Mhagama azindua kituo cha kwanza Tanzania cha Mafunzo ya Umahiri wa Tiba ya Magonjwa ya Dharura BMH




**Kituo** cha Ujuzi (Tanzania Emergency Care Training Center) kwa ajili ya tiba ya magonjwa ya dharura kimezin duliwa katika Hospitali ya Benjamin Mka pa (BMH) ili kuongeza ujuzi kwa watoa huduma za afya katika mikoa mbalimbali nchini. Akizundua Kituo hicho Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, amesema kituo hicho ni muhimu wakati nchi inapoelekea kuandaa mashindano ya AFCON,2027 ili kuandaa watoa huduma za dharura kati ka mashindano hayo.

Aidha, Mheshimiwa Mhagama aliele za dhamira ya Serikali ya kuifanya BMH kuwa Hospitali ya pili ya Taifa hivyo Menejimenti haina budi kuhakikisha mnasonga mbele. Waziri Mhagama azindua kituo cha kwanza Tanzania cha Mafunzo ya Umahiri wa Tiba ya Magonjwa ya Dharura BMH 12 "Kituo hiki kitasaidia kupunguza vifo kwa kuwezesha watumishi wa afya kuongeza ujuzi," amesema Waziri wa Afya wakati akizundua Kituo hicho cha Mafunzo ya Magonjwa ya Dharura kili chojengwa kwa ushirikiano na Shirika la ABBOT Fund.

Mwakilishi wa ABBOT Fund, Henry Sawe, amesema kuwa katika Kanda ya Kati kituo cha ujuzi kimejengwa katika Hospitali ya Benjamin Mkapa. "Leo ni siku ya muhimu sana katika huduma ya afya kutokana ushirikiano wetu na Serikali ya Tanzania kwa kuk abidhi kituo cha Mafunzo ya Magonjwa ya Dharura" amesema.

Ndugu Sawe amesema ABBOT Fund wamejenga zaidi ya vituo vya dharura 100 nchi nzima hivyo kuokoa vifo vya watan zania zaidi ya asilimia 40. Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Saitori Laizer ameipongeza Hospitali ya Benjamin Mkapa kwa kuanzisha kituo cha ujuzi (Tanzania Emergency Care Training Center).

"Wanafunzi wanaosoma kuhusu afya UDOM (University of Dodoma) wana weza kuja kusomea ubingwa na ubingwa bobezi hapa Hospitali ya Benjamin Mka pa," amesema Kaimu Katibu Mkuu wa Afya, Saitori Laizer.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Prof. Abel Makubi, alieleza kuwa kituo hicho kimegharimu TZS million 460, na kitaweza kutoa mafunzo kwa watalaamu 20 kwa wakati mmoja. Kituo hicho kinat egemewa kusaidia kutatua upungufu wa watalaamu wa tiba ya magonjwa ya Dharura katika ngazi ya afya ya msingi na wenye nia ya kujiendeleza katika umahiri wa eneo hilo. Prof Makubi alishukuru sana uwekezaji huu uliofanywa na Serikali ya awamu ya Sita chini ya Mhe Rais Samia Suluhu Hassan.



# Wauguzi BMH wadhamiria kufanya kazi kwa kujituma pamoja ili kuboresha huduma za tiba

**Ili** kuongeza ufanisi katika kutoa huduma, wauguzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) wamekubaliana kufanya kazi kama timu na kwa kujituma zaidi wanapohudumia wagonjwa.

Wameyasema hayo wakati wakiongea na Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Prof. Abel Makubi, katika kikao cha kufahamiana na kushirikishana mwelekeo wa Hospitali na dhana ya ubora wa huduma za tiba. Muuguzi Ndg Moabu Thobias kutoka CCU ameshauri kuwe na ushirikiano kati ya wauguzi na madaktari wanapozungukia wagonjwa wodini, na kuheshimiana kila mmoja.

"Nashauri kuwe na kufanya kazi kwa pamoja kati ya madaktari na wauguzi wanapowazungukia wateja ili kuongeza ufanisi wa kutoa huduma," amesema Ndg. Thobias. Ndg. Matuga Mwamtende, muuguzi kutoka Kliniki ya Damu, ameshauri BMH kuanzisha kliniki ya huduma mkoba ku saidia kutoa elimu kwa wananchi juu ya huduma inayotolewa na kliniki husika.

"Tuwe na Huduma mkoba ya kliniki ili kutoa elimu kwa wa nanchi kuhusu magonjwa yanayotibiwa na kliniki husika," amesema. Wamesema madaktari wanapowazungukia wateja wodini, mbali ya madaktari kuambatana na wauguzi, lakini pia timu ya watoa huduma iambatane na wafa masia na wataalamu wa maabara.

"Naomba tuwe tunazungukia wagonjwa shirikishi wodini kwa kushirikiana na wafamasia, wataalamu wa maabara na madaktari," amesema Sr. Eveline Omire.







# BMH washirikiana na Madaktari Bingwa kutoka Uholanzi kufanya upasuaji wa moyo kwa zaidi ya siku 22



**Wananchi** wanaosumbuliwa na matatizo mbalimbali ya moyo wamejitokeza kwenye kambi ya moyo ambayo ilianza Septemba 30 mpaka 20 Oktoba 2024 Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) Prof Abel Makubi, Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, akiongea wakati wa ufunguzi wa Kambi hiyo ya moyo, amesema wanafanya matibabu ya moyo kwa kufungua kifua kwa watu wenye magonjwa ya moyo kwa kushirikiana na madaktari bingwa kutoka Uholanzi.

"Kwa hiyo watanzania wanaosumbuliwa na matatizo ya moyo ni muhimu kutumia fursa hii ya matibabu yan ayo patikana hapa BMH waje wafanye uchunguzi ili wapate matibabu ikiwemo upasuaji wa moyo na kifua," amesema Prof. Makubi

Ameongeza kuwa wataalamu hao wa magonjwa ya moyo kuto ka Uholanzi wametoa vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya milioni 450 na kwamba vifaa hivyo vitawezesha kuwa hudumia wananchi wengi watakao kuja kupata matibabu ya moyo.

Kwa mujibu wa Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo, John Meda, watu wanaosumbuliwa na ugonjwa wa kisukari, shinikizo la damu, figo, kiharusi wanapaswa wahudhurie kliniki ya moyo kwa kuwa baadhi yao huwa sehemu za moyo zimeathirika pia.

Aidha, Dkt. Ahmed Toure Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Moyo ameeleza kuwa kuwepo kwa huduma za matibabu ya moyo kanda ya kati kunatoa fursa ya kupunguza adha kwa wananchi kusafiri umbali mrefu kupata matibabu hayo ambapo mpaka sasa BMH ime jiimarisha katika tiba ya Moyo.

"Kwa mujibu wa matibabu ya moyo inatutaka kila palipo na wananchi milioni mbili kuwe na kituo cha matibabu ya Moyo, hivyo Serikali ya awamu ya sita inaendelea kuwekeza katika matibabu ya Moyo ili wananchi wengi zaidi wapate huduma kwa ukaribu" amesema Dkt. Toure.

Daktari huyo alieleza kutokana na ongezeko la watu kufika zaidi ya Milioni 60 kwa watanzania, changamoto za magonjwa yasiyoambukiza na kuongezeka kwa umri wa mtanzania kuishi, kuna haja kama nchi kuwa na Hospitali zaidi za kutibu magonjwa ya moyo, ambapo inashauriwa katika kila watu milioni mbili ni vema kuwa na Kituo cha matibabu ya moyo.

Kwa upande wake kiongozi wa madaktari bingwa wa Moyo kutoka Uholanzi, Grandjean Gerhard Jan, amesema ushirikiano kati ya madaktari bingwa wa moyo wa Tanzania na Uholanzi umekuwepo kwa miaka kadhaa sasa.

"Nashukuru ushirikiano huu umesaidia kubadilishana uzoefu na wenzetu wa Tanzania," amesema Bw. Gerhard Jan.

Timu ya madaktari bingwa wa moyo 10 ambao wametoka Shirika la ZGT Overzee kutoka Uholanzi wanashirikiana na wenzao wa BMH katika kambi hiyo ya moyo iliyoanza mwisho wa mwezi Septemba mpaka Oktoba 21, 2024.

# Wagonjwa 762 wahudumiwa na Madaktari Bingwa kutoka BMH kwa kutumia Magari Tembezi yenye Vyumba vya Upasuaji Zanzibar

**Wananchi** wa Zanzibar wamenufaika na kambi ya madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma iliyo tolewa mwezi Septemba ambapo jumla ya wagonjwa 762 wamepata uchunguzi na matibabu katika magonjwa ya mfumo wa mkojo, magonjwa ya ubongo na mishipa ya fahamu, magonjwa ya mifupa, magonjwa ya moyo, magonjwa ya ndani na macho.

Waziri wa Afya Mhe. Nassor Mazrui wakati akihitimisha kambi maalumu ya magari yenye vyumba vya upasuaji (theater) alitoa shukrani kwa madaktari Bingwa na Wataalamu waliotoa huduma Zanzibar na hususani katika Hospitali ya Mwerapongwe

"Naifunga kambi hii nikitambua imetupa faida nyingi kwanza wananchi wa pembezoni wamepata huduma za matibabu na upasuaji, pili mmewajengea uwezo wataalamu wetu na tatu kwakuleta magari haya nasi tunaonakunahaja ya kuwa nayo hivyo tutafan ya tathimini ya kuona uwezekano wa kuwa na magari kama haya," amesema Mhe. Mazrui



Ameongeza kuwa sasa imefika wakati wa kurasimisha mahusiano baina ya Zanzibar na Hospitali ya Benjamin Mkapa.


"Kabla ya mwezi Disemba lazima tuje kuitembelea Hospitali ya Benjamin Mkapa, nia ni kuiona na pia kuingia makubaliano rasmi na Hospitali ya Benjamin Mkapa ambayo yatabore sha huduma za kibingwa, mafunzo na kubadilishana uzoefu na wataalaamu," amesema Mhe. Mazrui

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji Hospitali ya Benjamin Mkapa Prof. Abel Makubi amezishukuru sana serikali za JMT na SMZ kwa kuruhusu kambi hiyo na kuwapokea watalaamu, kuandaa mazingira mazuri na mwitikio wa wananchi ulikuwa mkubwa sana.

"Mpaka tunapohitimisha tumeona wananchi 762 na kati ya hao 60 wamefanyiwa upasuaji na wengine wamepata matibabu, kambi hii imeku wa na msaada kwa wakazi wa Zanzibar," amesema Prof. Makubi.

Aidha, baadhi ya wagonjwa walimuomba Mheshimiwa Waziri wa Afya kuona namna ya kuongeza muda wa kambi hizo kwa siku zijazo ili wananchi wengi wanufaike. Huduma za upasuaji ubingwa za ubongo, mifupa, macho na njia ya mkojo zilitolewa kwa wananchi walioko pembezoni mwa mji wa Unguja.

Aidha, Prof. Makubi ameeleza nia ya kuja kutoa huduma Zanzibar ni kutoa huduma kwa wananchi wa Zanzibar na bara, na kuwajengea uwezo madaktari na wataalamu wa Hospitali za hapa Zanzibar. Kambi hii ya magari maalumu yenye vyumba vya upasuaji (theater) imeanza kutoa huduma Zanzibar kisha itakwenda Dodoma, Kigoma na Burundi.




# BMH, UDOM kushirikiana na Japan kujenga Kituo cha Umahiri cha Upandikizaji Figo na kuanzisha Shahada ya Uhandisi Vifaa Tiba

**Mhe. Baraka Luvanda,** Balozi wa Tanzania nchini Japan, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Prof. Abel Makubi na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Prof. Lughano Kusiluka kwa pamoja wametembelea Makao Makuu ya Shirika la Tokushukai, jijini Tokyo na kukutana na Mwenyekiti wa Shirika hilo, Prof. Shinichi Higashiue.

Katika mkutano huo, viongozi hao walikubaliana kuanza mchakato wa mradi wa ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Tiba, mafunzo na Tafiti za upandikizaji wa Figo kitakachojengwa jijini Dodoma.

Kituo hicho kitaendeshwa kwa ushirikiano kati ya Hospitali ya Benjamin Mkapa na Chuo Kikuu cha Dodoma. Aidha, katika kikao hicho walijadili kuanza matumizi ya teknolojia ya "robotics" katika upandikizaji figo na upasuaji wa ubongo nchini Tanzania.

Shirika la Tokushukai limeahidi kutoa fedha kwa ajili ya mradi huo ambao unatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwaka 2025.

Aidha, watendaji wa taasisi hizo mbili wamekutana na Prof. Shuzo Kobayashi, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Shonan Kamakura, ambayo ina kituo kikubwa cha usafishaji damu pamoja na teknolojia za kisasa za tiba ya saratani kwa kutumia "Proton Beam Therapy" na "Boron Neutron Capture Therapy". Prof. Kobayashi pamoja na Prof. Tanabe Kazunari ni waanzilishi wa huduma ya upandikizaji figo jijini Dodoma ambayo ilihusisha wataalamu wa Chuo Kikuu cha Dodoma na Hospitali ya Benjamin Mkapa mwaka 2018 baada ya kupata mafunzo nchini Japan.

Ziara hiyo iliwakutanisha watendaji hao na viongozi wa AFRECO ambacho ni Chama cha Maendeleo ya Uchumi wa Afrika nchini Japani pamoja na taasisi ya Japani ya Ukuzaji wa Tasnia ya Uhandisi wa Vifaa Tiba ikiwa ni juhu di za kupata wataalamu na vifaa kwa ajili ya kuanzisha mafunzo ya Shahada ya Uhandisi wa Vifaa Tiba katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

# BMH yafanikiwa kupandikiza uloto kwa mtoto aliyeshindikana barani Asia




**Mama** wa mtoto aliyepatiwa matibabu ya upandikizaji uloto Bi. Shani Mgaraganza amesema anamshukuru sana Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuanzisha huduma hizi za matibabu ya upandikizaji uloto.

"Mwaka 2023 tulienda Asia kupata matibabu ya upandikizaji uloto, tulifanikiwa kupata matibabu lakini mtoto hakuonesha kupona. Kupitia Wizara ya Afya nilipatiwa msaada wa kurudia tena matibabu hayo hapa Hospitali ya Benjamin Mkapa. Namshukuru Mungu mtoto ameruhusiwa akiwa na matokeo makubwa zaidi hadi madaktari wa Asia wamehitaji kujua utaalamu uliotumika hapa Hospitali ya Benjamin Mkapa," alisema Shani.

Kwa upande wake, Daktari William Lloyd ameelezea mchakato wa matibabu ya mtoto huyu yamewapa hatua nyingine ya matibabu.

"Kwa kawaida, binadamu wa kawaida ana chembe sahani kuanzia 200. Mtoto huyu alikuja na chembe sahani 1, jopo la madaktari limefanikiwa kumpandikiza uloto ambao uliendelea kuzalisha chembe sahani na mpaka tunamruhusu zimefikia 57, hii ni hatua kubwa tuliyoifikia" alisema Dkt. Lloyd.

Matibabu ya upandikizaji uloto yalianza kutolewa mwanzoni mwa mwaka 2023, na kuwa yanaipa alama ya juu ya utoa ji matibabu ya aina hii hapa Tanzania na katika ukanda huu wa Afrika Mashariki kwa kuwa nchi pekee inayotoa matibabu haya.



# BMH yavuna figo kwa upasuaji matundu madogo kwa mara ya kwanza

**Madaktari** Bingwa na Wataalamu wa Hospitali ya Benjamin Mka pa (BMH) kwa kushirikiana na Madaktari Bingwa kutoka Shirika la ZGT Overzee la Uholanzi, wamefanikiwa kuvuna figo kwa mtu (jina limehifadhiwa) kwa kufanya upasuaji wa matundu madogo zoezi lina lojulikana kitaalamu kama Laparoscopic Nephrectomy figo hiyo ikivunwa inakwenda kupandikiza kwa Mgonjwa wa Figo.

Hii ni mara ya kwanza kwa BMH kuvuna figo kwa njia ya matundu madogo kutoka kwa mtu ambaye anamchangia figo ndugu yake mwenye tatizo la figo na kisha kupandikiza kwa mgonjwa mwenye tatizo la figo, huduma ya upandikizaji figo ina miaka sita tangu ianzishwe Hospitali ya Benjamin Mkapa.

BMH ilikuwa ni Hospitali ya pili ya Umma kuanzisha huduma ya upandikizaji figo mwaka 2018. Aina hiyo ya matibabu ya Laparoscopic Nephrectomy imefanyika hospitalini hapo kwenye kambi maalum ya matibabu ya Madaktari Bingwa wa BMH wanaoshirikiana na Madaktari Bingwa kutoka Uholanzi.

Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Prof Abel Makubi, amesema kuwa huduma hiyo haihusishi kumfanyia upasuaji mtu anaemchangia figo Mgonjwa wa figo badala yake figo inatolewa kupitia kitundu kidogo. Ametaja faida ya huduma hiyo kuwa ni kumpunguzia muda wa kukaa Hospitali mchangiaji figo.

"Unapovuna figo kwa njia ya matundu madogo inamsaidia mchangiaji kutotumia dawa nyingi, hivyo inapunguza gharama za dawa na matibabu ya mchangiaji wa figo," amesema Mkurugenzi Mtendaji wa BMH

Kambi ya Matibabu ya Madaktari Bingwa wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) kwa kushirikiana na madaktari bingwa wa shirika la ZGT Overzee la nchi ni Uholanzi imewahudumia wananchi wa kanda ya kati ambapo jumla ya Wagonjwa 18 Katika wagonjwa hao 18, mmoja (1) amefanyiwa matibabu ya upandikizaji wa Figo, nane (8) wamefanyiwa upasuaji wa magonjwa ya wanawake na wengine tisa (9) wamefanyiwa upasuaji wa jumla (General Surgery).

# Ujumbe kutoka Wizara ya Afya Somalia wapata uzoefu wa mnyororo wa dawa na vifaa tiba katika Hospitali ya Benjamini Mkapa

**Ujumbe** wa watu nane (8) kutoka serikali ya Somalia umetembelea Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) jijini Dodoma kujionea mnyororo wa ugavi wa dawa kutoka Bohari ya Dawa (MSD) mpaka Hospitalini.

Kiongozi wa ujumbe huo kutoka Somalia, Mkurugenzi wa Ugavi kutoka serikali ya Somalia, Ndg. Mohamed Hersi, amesema lengo la ziara hiyo ni kujifunza kutoka serikali ya Tanzania inavyoratibu shughuli za ugavi wa dawa.

"Tumekuwa na ziara nzuri, tumejifunza kuhusu ugavi wa dawa kutoka bohari ya dawa (MSD) mpaka zinapomfikia mgonjwa katika famasi ya hapa Hospitali," amesema Ndg.Hersi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Prof Abel Makubi, ameushukuru ujumbe huo kwa kutembelea BMH.

"Naishukuru Wizara ya Afya kwa kuichagua Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) kuwa moja ya taasisi za kuja kujifunza kwa ujumbe huu na tuna furaha kuwapokea," amesema Prof. Makubi.

Aidha, Mfamasia wa BMH Ndg. Amani Msami, akiwasilisha andiko kuhusu mnyororo wa ugavi wa dawa, amesema uchaguzi wa dawa zinazopaswa kusambazwa BMH unafanywa na Idara ya Famasi.



# Mambo muhimu ya kuzingatia tunapoelekea zama za kidigitali




**Watumishi** wa Hospitali ya Benjamin Mkapa wametakiwa kuzingatia mambo muhimu katika kuelekea zama za kidigitali ambayo ni mtazamo, kufanya kazi kwa ushirikiano, kuwa na umiliki wa taasisi, mawasiliano na mrejesho wakati wa kutoa huduma.

Wito huo umetolewa katika mafunzo endelevu (continuous medical education-CME) na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH), Prof Abel Makubi, amesema mambo hayo ni muhimu kufanyika kwani yatawezesha BMH kupata ithibati.

"Turudi katika misingi ya taaluma zetu tuliyofundishwåa. BMH imeendelea kutoa huduma bora, hata hivyo tunahitaji ziwe bora zaidi ya sasa ili BMH iweze kufikia lengo la kuwa Hospitali ya taifa," amesema Prof. Makubi.

Katika misingi ya taaluma ya udaktari, Prof. Makubi amefafanua kuwa mgonjwa anapofika kwa daktari, daktari anapaswa kujitambulisha, kumsikiliza mgonjwa halafu kumpima na kumpa mrejesho kwa wakati.

Mkurugenzi Mtendaji wa BMH ameendelea kueleza kuwa watalaam wa afya sasa wanahitaji  kubadili mtazamo katika utaoaji wa huduma kwa kuwa tayari  kumsikiliza mgonjwa na kumhusisha katika matibabau yake badala kumuandikia tu vipimo na dawa bila kutoa ufafanuzi wa hatua za matibabu.

Vile vile Prof. Makubi ameongeza kuwa baadhi ya magonjwa yanahitaji ushirikishwaji wa watalaamu wengine ili kutoa huduma bora na zenye manufaa kwa mgonjwa kwani kuna shida nyingine zinahitaji watalaamu zaidi ya mmoja wenye ujuzi tofauti.

Jambo lingine lililosisitizwa ni watumishi kuwa na umiliki wa taasisi ikiwa pamoja na kutimiza majukumu yake kwa wakati bila kusukumwa na  kutunza mali za Hospitali, Prof. Makubi amefafanua zaidi kuwa lazima kila mtumishi afikie malengo ya kutoa huduma bora kwa wakati.







# Madaktari wapya watakiwa kufuata utamaduni wa BMH

**Mkurugenzi** Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH), Prof. Abel Makubi awataka madaktari wapya 16 waliopata ajira kufuata utamaduni wa BMH.

"Unapoingia kwenye jamii yoyote ni lazima uangalie wanaishi kwa namna gani kama wanaamka asubuhi basi nawe unaamka asubuhi, hivyo nanyi lazima mjue kuna utamaduni wa BMH lazima muendane na tamaduni zetu," amesema Prof. Makubi.

Prof. Makubi amewataka madaktari hao kuwa hudumia wagonjwa katika viwango vya juu kwani BMH inaelekea kuwa hospitali ya taifa.

"BMH inaelekea kuwa hospitali ya taifa hivyo tuhudumie wagonjwa kama hospitali ya taifa, tuwe na utashi wa kudadavua mambo na tubadili mitazamo yetu tuvae viatu vya mgonjwa kwa kutoa huduma bora," ameeleza Prof. Makubi.

Prof. Makubi ameendelea kuwataka madaktari hao wafanye uchunguzi wa kina kwa mgonjwa pindi anapokuja BMH kupata huduma.

"Mgonjwa akija hapa mfanyieni uchunguzi wa kina maana ametoka huko amekuja hapa hivyo Hospitali inatakiwa kumchunguza kwa kiwango anacho stahili kwa hiyo matibabu na uchunguzi hapa siyo basic ni comprehensive medicine," ameongeza Prof. Makubi.

Akiendelea kuzungumza Prof. Makubi amewataka madaktari hao kuwa na ushirikiano wa karibu na watumishi wengine wa kada za afya kwani itaongeza ufanisi kwenye kutoa huduma.

"Niwaombe muwe na ushirikiano wa karibu na kuheshimiana na wauguzi, wafamasia na wataalam wa maabara ili kuweza kutoa huduma bora kwa wagonjwa," ameeleza Prof. Makubi.

# Mambo 9 muhimu katika kujenga utamaduni wa kazi kwa Watumishi wa BMH

**Mambo 9 muhimu** yametajwa kwa ajili ya kujenga utamaduni kwa Watumishi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) wanapo hudumia wagonjwa na watumishi wenzao.

Akifungua mafunzo ya kuzidhibiti msongo wa mawazo na Huduma kwa mteja, Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Prof. Abel Makubi, amesema mambo 9 muhimu yatafanya mgonjwa aje Hospitali ya Benjamin Mkapa anapotaka huduma bora .

"Sio kama namaanisha watu waugue lakini namaanisha katika jamii mtu akiumwa achague kuja Hospitali ya Benjamin Mkapa kupata huduma bora," amesema Prof. Makubi

Mafunzo hayo yameshirikisha washiriki kutoka mapokezi, walinzi, wahasibu, wauguzi, madaktari na mafundi.

Prof. Makubi ametaja mambo hayo 9 muhimu kwa ajili ya kujenga utamaduni wa huduma kwa mteja kuwa ni kubadili msimamo akiongeza

"Msiwe wagumu kubadilika kwenda mwelekeo chanya maana mkibadilika ni manufaa kwa wagonjwa na nyinyi wenyewe", alisema Prof. Makubi.

Ametaja jambo jingine kuwa ni kuitumia kauli mbiu yetu ambayo ni "Kuvaa viatu vya mgonjwa, uwajibikaji na kujituma" kwa kutoa huduma bora na kuonesha kwa matendo kweli jigeuze kuwa mgonjwa ili umuhudumie kama wewe.

Prof. Makubi amefafanua kuwa lugha iwe njema kwa wagonjwa tuweke mbele maneno haya Pole, Samahani, naomba nikusaidie, na kuepuka kuchelewesha huduma au kuzungusha mgonjwa.

"Tuwe na umiliki wa taasisi tujue huyu ndiyo mama yetu anatulipa stahiki zote tumtendee haki ili tuwatumikie wagonjwa wanaokuja na tusikubali taasisi yetu kutoa huduma mbovu au idhalilike na tuipiganie popote pale.

Prof. Makubi ametaja uwajibikaji kuwa ni jambo jingine kujenga utamaduni wetu na ni lazima ujipime unafanya nini kwenye muda unaokuja ofisini unafanya nini? Unakuja umechelewa halafu haujiulizi wala haushtuki kwanini hautumii muda wako vizuri kuhudumia Wananchi.

"Huduma kwa wateja iwe ni ya kuvutia na wepesi wa kumuhudumia mgonjwa, mgonjwa akimaliza kupata huduma aridhike," ameongeza.

# Watoto 21 wafanyiwa upasuaji wa moyo BMH

**Watoto 21** wenye matatizo ya moyo wamenufaika na matibabu ya moyo kwa njia ya kufungua kifua katika kambi maalumu iliyofanywa na Madaktari Bingwa kutoka Kuwait wakishirikiana na Madaktari Bingwa wa Hospitali ya Benjamin Mkapa iliyofanyika tarehe 21 mpaka 28 Februari BMH.

Akiongea na waandishi wa habari kuhusu matokeo ya kambi ya pamoja ya matibabu ya moyo kwa watoto iliyotekelezwa na BMH na madaktari Bingwa wa moyo kutoka Shirika la Children Heart Association la Kuwait. Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Prof. Abel Makubi, amesema watoto wa watanzania wamenufaika na kambi hii kwa kupata matibabu ya kudumu.

"Ni mshukuru Mhe. Rais Samia kwa kuendeleza ushirikiano baina ya Tanzania na Kuwait, mashirikiano haya yanatupatia manufaa kwa Wataalamu wetu kuendelea kujengewa uwezo na kuongeza wigo wa matibabu kwa wagonjwa wenye matatizo ya moyo," amesema Prof. Makubi.



Timu ya wataalamu wa magonjwa ya moyo kumi na sita (16) kutoka Shirika la Children Heart Association la Kuwait wanafanya kambi kwa pamoja ya matatizo ya moyo kwa watoto na madaktari bingwa wa moyo wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) ya jijini Dodoma.

Prof. Makubi ametaja dalili za matatizo ya moyo kwa watoto kuwa ni kupumua kwa shida, kikohozi cha mara kwa mara, mtoto kushindwa kunyonya na kutokwa na jasho jingi wakati wa usiku na kutoongezeka uzito.

"Dalili nyingine kwa mtoto mwenye matatizo ya moyo ni kupata fatigue (kuchoka sana) na kushindwa kuhimili mazoezi," amesema Prof. Makubi.

Prof. Makubi ametumia fursa hiyo kuwashukuru timu ya wataalamu wa moyo kutoka Kuwait kwa ushirikiano na BMH na ushirikiano huo ulianza mwaka 2023 na mwaka 2024 BMH ikasaini makubaliano na Shirika hilo la Children Heart Association.

Kwa upande wake, kiongozi wa msafara wa timu ya wataalamu kutoka Kuwait, Prof. Faisal Al-Saidei, amesema lengo la wao kushirikiana na BMH ni kutoa matibabu ya moyo kwa watoto waliozaliwa na matatizo ya moyo.

"Pamoja na kufanya kambi ya pamoja ya matibabu ya moyo kwa watoto pia tunajenga programu ya ushirikiano na Hospitali ya Benjamin Mkapa," amesema Prof. Al-Saidei.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Tiba wa BMH, Dkt. Kessy Shija, magonjwa ya moyo kwa watoto yanaweza kuchangiwa na magonjwa yasiyo ya kuambukiza na maambukizi kwa wazazi au mtoto.









# Wataalam BMH watakiwa kuitumia Bodi ya Matibabu ya Ugonjwa wa Saratani (Multidisciplinary Tumor Board)

**Madaktari,** Wauguzi na Wataalamu wa Maabara wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) wametakiwa kutumia Bodi mtambuka ya matibabu ya ugonjwa wa saratani kwa lengo la kuweza kutoa matibabu sahihi na bora kwa wagonjwa wa saratani.

Wito huo umetolewa katika Mkutano wa mafunzo endelevu na daktari kutoka Idara ya Saratani (BMH), Dkt. Gideon Abisai, ambaye amesema Bodi hii inahusisha wataalam kutoka katika kada na taaluma mbalimbali za udaktari kwa ajili ya kujadili na kutoa uamuzi kuhusu matibabu sahihi ya kumpatia mgonjwa wa saratani.

"Timu hii inahusisha madaktari bingwa wa magonjwa ya uvimbe na saratani, madaktari bingwa wa magonjwa ya tumbo, madaktari bingwa wa mionzi, madaktari bingwa wa mishipa ya fahamu na ubongo, wataalam wa dawa, wataalam wa afya ya akili na wauguzi wabobezi ili kuweza kujadili matibabu ya mgonjwa wa saratani, hivyo ushauri wake ni muhimu kwa matibabu sahihi kwa mgonjwa" amesema Dkt. Abisaih.

"Kupitia timu hiyo itaweza kusaidia kupunguza muda wa mgonjwa kusubiria majibu kutoka kutolewa sampuli ya ugonjwa mpaka kuanzishwa kwa matibabu ambayo yanazingatia miongozo ya kitaaluma kwa sababu ya uamuzi wa matibabu kufanywa na madaktari zaidi ya mmoja", ameongeza Dkt. Abisaih.

Daktari bingwa wa magonjwa ya saratani, Dkt. Jesse Kashabano amewashauri madaktari kuweza kutumia Timu hiyo ya wataalam ili kuweza kutoa matibabu sahihi.

"Nawashauri madaktari kuweza kutumia hizi Timu za Madaktari kwani zinasaidia mgonjwa kupata matibabu ya usahihi na itasaidia mgonjwa kupunguza gharama ya kupata tiba chini ya viwango" amesema Dkt. Jesse

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa mafunzo na huduma mkoba, Dkt. Sylivia Jumbe amesema tukitumia vizuri Timu hii ya wataalam itatusaidia kuboresha matibabu ya wagonjwa wa saratani na kuanza matibabu mapema pindi mgonjwa anapogundulika na tatizo.

# BMH yapokea viti mwendo 30, medical oxygen concentrator 4 vyenye thamani ya milioni 28

**Hospitali** ya Benjamin Mkapa (BMH) imepokea viti mwendo 30 na medical oxygen concentrators 4 vyenye thamani ya milioni 28 kutoka mdau wa Afya kutoka Dar es Salaam.


Akipokea msaada huo, Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Prof. Abel Makubi, ameahidi msaada utatumika kwa wagonjwa kama ilivyokusudiwa.

"Leo, tumepata mdau kutoka Dar es Salaam ambaye amekuja kutuunga mkono. Tunaahidi misaada hii itatumika kama ilivyokusudiwa kwa wagonjwa," amesema Mkurugenzi Mtendaji.

Kwa upande wake, mdau wa Afya, Mzee Akhter Khakoo, amesema ametoa msaada huo kwa kushirikiana na familia yake.

"Bado nitaendelea kutoa misaada kama hii kwa Hospitali za umma kwa kushirikiana na familia yangu," amesema Mzee Khakoo.







# Balozi wa Italia afuraishwa na huduma za Upandikizaji Uloto zinavyoendelea BMH

**Balozi** wa Italia nchini Tanzania, Mhe. Giuseppe Cuppola, alipotembelea Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) kuelezea kuridhishwa na huduma ya upandikizaji uloto ambayo iliianzishwa kwa kushirikiana na Italia.

Alipokuwa akiongea na uongozi wa BMH, Mhe. Balozi Coppola, alisema msaada huo ni ishara ya mahusiano mazuri kati ya Tanzania na Italia.

"Sekta ya Afya ni mojawapo ya sehemu ambayo tumekuwa tukishirikiana na Tanzania katika kutoa huduma za upandikizaji uloto, hii inaonesha kuwa tuna mahusiano makubwa baina ya Italia na Tanzania," amesema Mhe. Balozi Coppola.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Prof. Abel Makubi, alimshukuru Mhe. Balozi Coppola kwa msaada wa kusaidia kuanzisha huduma ya Upandikizaji Uloto BMH.

"Leo, tunafurahi kukupokea kuja kujionea huduma ya upandikizaji uloto ambayo Serikali ya Italia ilifadhili uanzishwaje wake. Tunashukuru na kuthamini msaada huu uliotokana na mashirikiano mazuri kati ya Italia na Tanzania," amesema Prof. Makubi.

Mkuu wa Idara ya magonjwa ya damu, Dkt. Stella Malangahe, alisema madaktari na wauguzi kutoka BMH walifaidika kupitia mafunzo nchini Italia.

"Mpaka sasa, tumeshapandikiza uloto kwa watoto 19 toka tulipoanza huduma mwaka 2023," amesema Dkt Stella.

Aidha, mwakilishi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Dkt. Missama Yango, ameishukuru Serikali ya Italia kwa miradi mbalimbali ambayo inayotolewa kwa Dodoma na Kanda ya Kati kwa ujumla.

"Kanda ya Kati ni wanufaika wa miradi mbalimbali inayofadhiliwa na Serikali ya Italia katika sekta ya Afya. Naishukuru Serikali ya Italia kwa kusaidia kuanzisha huduma ya upandikizaji uloto hapa BMH," amesema Dkt. Yango.





# Menejimenti ya BMH yapigwa msasa masuala ya Uongozi, Usimamizi



**Menejimenti** ya Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) imepigwa msasa kwenye masuala mazima ya uongozi na usimamizi kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Akifungua mafunzo hayo Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Prof. Abel Makubi ameitaka menejimenti kuwa na uelewa mmoja katika kutafsiri maono na mpango mkakati wa Taasisi kama viongozi katika kuboresha huduma.

"Tumeona ni vema menejimenti yote kwa pamoja na baadhi ya watumishi kushirikishana, kueleweshana na kubadilishana uzoefu katika kutekeleza maono ya BMH ambayo yalitafsiriwa kwenye vipaumbele vyetu ili tuweze kutoa huduma bora kwa wananchi," amesema Prof. Makubi.

Prof. Makubi ameendelea kwa kuwataka viongozi kuwa na uelewa wa pamoja ambao utasaidia katika kufanya kazi kwa pamoja na kuwa na uelekeo mmoja.

"Tukiwa na uelewa wa pamoja itasaidia katika kujenga timu ya pamoja na kuwa katika mstari mmoja na hii itasaidia katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku," ameendelea Prof. Makubi.

Prof. Makubi ameitaka mafunzo haya yakaleta mtazamo chanya na kuwezesha kubadilisha mitazamo yetu ili iweze kuleta mabadiliko katika Taasisi yetu ya BMH.

"Mafunzo haya yatatujengea mtazamo mpya ambao ni chanya na kubadilika kuelekea kwenye mazuri zaidi hivyo kama viongozi tutumie ushawishi wetu ili kufikia maono ya Taasisi," ameongeza Prof. Makubi.

Aidha, Prof. Makubi aliwataka viongozi hao kushusha mafunzo haya kwa watumishi waliopo chini yao ili kuboresha huduma za BMH.

"Naomba Mafunzo haya muwasilishe kwa wakuu wa maeneo na watumishi wenzetu angalua kuwe na mafunzo mafupi ya kuwajengea uwezo ili kuboresha huduma na kuwa na uelekeo mmoja," ameeleza Prof. Makubi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Utawala na Rasiliwatu, Bw. Teophory Mbilinyi amewataka viongozi hao kuwa na umiliki wa BMH na uzalendo katika kuhudumia wananchi.

"Tukifanya kazi BMH lazima tuwe na umiliki wa BMH na uzalendo katika kuboresha huduma na kuwahudumia wananchi," amesema Bw. Teophory.




*Watumishi wanawake wa BMH wakiwa kwenye maandamano ya siku ya Wanawake Jijini Arusha*

# Waziri Mhagama: Hospitali za umma nchini anzeni kutumia simu za upepo ili kupunguza matumizi ya simujanja kazini




**Waziri** wa Afya Mhe. Jenista Mhagama amezitaka Hospitali za mikoa hadi Taifa nchini kuanzisha mfumo wa matumizi ya simu za upepo ili kupunguza matumizi ya simu za mkononi ambazo hazina tija kwenye utoaji wa huduma bora kwa wananchi wakati wa muda wa kazi.

Waziri Mhagama ameyasema hayo jijini Dodoma wakati wa uzinduzi wa miradi katika Hospitali ya Benjamin Mkapa. Amesema simu hizo zitasaidia uwajibikaji wa watumishi wa sekta ya afya, kusaidia uratibu wa huduma kwa wateja na hata kugundua wa tumishi wasiokuwa katika eneo la kazi. Waziri Mhagama ameupongeza uongozi wa Hospitali hiyo chini ya Prof. Abel Makubi kwa ubunifu huo mzuri na utoaji wa huduma bora kwa wateja kupitia mbinu za kiteknolojia kuhakikisha wanawahudumia wagonjwa kwa ufanisi na kuleta tija

# BMH, Moran Eye Center ya Marekani wakubaliana kuijengea uwezo Idara ya Macho ya BMH

**Hospitali** ya Benjamin Mkapa (BMH) na taasisi ya Moran Eye Center ya Chuo Kikuu cha Afya cha Utah cha nchini Marekani wamekubaliana kuendeleza ushirikiano na kuendelea kuijengea uwezo Idara ya matibabu ya macho ya BMH.

Madaktari Bingwa wa Macho wa BMH kwa kushirikiana na madaktari Bingwa wa Moran waliweka kambi ya Uchunguzi wa magonjwa ya macho kwa wananchi iliyofanyika Machi 5 hadi 7, 2025 na kisha kufanya upasuaji wa macho kuanzia Machi 10 hadi 14, 2025.

Akitoa salamu za kuushukuru ujumbe huo kutoka Marekani, Prof. Makubi amebainisha kuwa ushirikiano uliopo kati ya BMH na Moran Eye Center utasaidia wataalamu wa pande zote mbili kujifunza kutoka kwa kila mmoja na kujengeana uwezo katika utaalamu wa matibabu ya macho, masuala ya utafiti, huduma za Afya Mkoba kwa jamii (outreach programme) hususani kwenye maeneo ambayo ni vigumu wananchi kuweza kufika kwenye vituo vya Afya na Hospitali kubwa.

"Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa msaada wa mashine na vifaa tiba ambavyo taasisi ya Moran Eye Center ilichangia katika idara ya matibabu ya macho ya BMH na ushirikiano ambao umeendelea kuwepo kati ya Taasisi zetu hizi mbili, utasaidia wataalamu wetu kuweza kujengeana uwezo na kubadilishana uzoefu katika maeneo ya matibabu ya macho, mafunzo kwa wataalamu, masuala ya utafiti na huduma za Afya Mkoba kwenye jamii" amesisitiza Prof. Makubi

Prof Makubi ametaja Dodoma kama moja ya Mikoa yenye kiwango kikubwa cha matatizo ya macho na kuongeza kuwa mpango wa Serikali ni kuifanya BMH kuwa na Idara ya macho yenye uwezo wa ubingwa wa juu kuweza kukabiliana na tatizo hilo ili wananchi wanaokuja kutibiwa macho wapate huduma za ubingwa wa juu wa matibabu ya macho.

# BMH ya kwanza katika sekta ya umma kufanya upasuaji wa jicho kwa njia ya matundu madogo

**Hospitali** ya Benjamin Mkapa imekuwa Hospitali ya kwanza katika sekta ya Umma kwa kufanya upasuaji kwa njia ya matundu madogo.

Mkuu wa Idara ya magonjwa ya macho Dkt. Jacinta Feksi amesema mpaka tunapo hitimisha kambi hii tumeona wagonjwa 1020 katika magonjwa mbalimbali ya macho.

"Jambo ambalo tunajivunia ni kuwahudumia wagonjwa wenye matatizo ya macho kwa njia ya upasua wa matundu madogo ili kuondoa mtoto wa jicho" amesema Dkt. Jacinta

Ameongeza kuwa njia hii inafaida kubwa kwa mgonjwa kiuchumi na kiafya.

"Hospitali ya Benjamin Mkapa itatoa matibabu haya kwa gharama ndogo ukilinganisha na maeneo mengine, hata hivyo njia hii humfanya mgonjwa kuhuruhusiwa mara baada ya upasuaji kufanyika" amesema Dkt. Jacinta

Kwa upande wake Daktari Bingwa wa magonjwa ya macho na mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma Frank Sandi ameeleza ushirikiano wa madaktari Bingwa wa macho kutoka marekani (Morani) ni wa muda mrefu unazaidi ya miaka tisa.

"Ushirikiano wa Chuo Kikuu cha UDOM, BMH na Morani unaleta matokeo chanya ya kuwa hudumia watanzania kwa teknolojia ya hali ya juu, lakini pia inawajengea uwezo madaktari na wataalamu wengine" amesema Dkt. Frank

Aidha kiongozi wa msafara wa madaktari Bingwa wa Macho Morani Dkt. Jeff Pettey amesema ni fahari kuwepo katika Hospitali ya Benjamin Mkapa na kuona jinsi wataalamu wanavyoendelea kuwahudumia wananchi.

"Tumekuja hapa mara kadhaa na kuona uwekezaji mkubwa uliofanyika lakini pia wataalamu walivyo na moyo wakutoa huduma hii inatupa nguvu ya kuendelea kuwa karibu na wataalamu wa Hospitali na Chuo Kikuu cha Dodoma" amesema Dkt. Jeff



# Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Ukimwi yaridhishwa na maendeleo ya ujenzi jengo jipya BMH

**Kamati** ya Kudumu ya Bunge ya Afya na masuala ya UKIMWI imeridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa jengo litakalokuwa Kituo cha Tiba mionzi kwa magonjwa ya saratani katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH).

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Ndg. Hassan Mtenga, amesema kituo hicho kitakapokamilika kitaipunguzia adha ya wananchi kusafiri umbali mrefu kwenda kutafuta matibabu ya saratani.

"Tunampongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa zaidi ya bilioni 30 kwa ajili ya ujenzi wa jengo hili, tulikuwa tunategemea Kituo kimoja tu, lakini jengo hili likikamilika kitapunguza adha ya wagonjwa kusafiri umbali mrefu kufuata matibabu," amesema Mhe. Mtenga.

Kamati hiyo ilitembelea ujenzi wa jengo hilo jipya katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) ikiwa sehemu ya kuitembelea miradi inayotekelezwa na Wizara ya Afya.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel, jengo hilo litakapo kamilika litakuwa ni Kituo cha Umahiri cha matibabu ya saratani kwa Afrika.

Dkt Mollel ametumia nafasi hiyo kumshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa zaidi ya bilioni 38 kwa ujenzi wa Kituo hicho.







# Kwa mara ya kwanza Hospitali ya Benjamin Mkapa yafanya operesheni ya ubongo kwa kutumia teknolojia ya mawimbi ya sauti





**Hospitali** ya Benjamin Mkapa (BMH) imefanikiwa kufanya upasuaji wa kwanza wa ubongo kwa kutumia Teknolojia ya mawimbi ya sauti na kufanikiwa kutoa damu yote iliyokuwa imevia kwenye ubongo wa mgonjwa.

Akizungumza na Kitengo cha Mawasiliano cha BMH Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu ambaye ndio aliongoza Jopo la Madaktari waliofanya Upasuaji huo wa kutumia Teknolojia ya Mawimbi ya Sauti Dkt. Maxigama Ndosi amesema kuwa walifanikiwa kutibu mvilio wa damu kwenye ubongo wa Mgonjwa kwa kusaidiwa na Mawimbi ya Sauti na kuitoa damu yote iliyovia kwenye ubongo.

"Hospitali ya Benjamini Mkapa imeanza kwa mara ya kwanza, matumizi ya Mawimbi ya Sauti kwa upasuaji wa kutoa damu na uvimbe kwenye ubongo teknolojia hii inasaidia kufungua sehemu ndogo ya kichwa na kumuacha Mgonjwa na kovu dogo ambalo linapona kwa haraka" amebainisha Dkt. Max.

Ameongeza kuwa utaalam wa kutumia mawimbi ya sauti utasaidia sana kupunguza muda wa upasuaji kwa wagonjwa ambao wana damu kichwani na hata wagonjwa wenye uvimbe ndani ya ubongo.

"Teknolojia hii inasaidia katika upasuaji wa ubongo wa kuondoa damu iliyovia kwenye ubongo kichwani au uvimbe kwa ajili ya saratani au wa namna nyingine na pia inaongeza ufanisi katika kufanya upasuaji wa aina yoyote ya ugonjwa ndani ya kichwa" amefafanua Dkt. Max.

Ameongeza kuwa Teknologia hii ni ya kipekee hivyo BMH itaanza kufanya upasuaji kwa njia hii ili kuongeza ufanisi wa upasuaji na kuondoa damu ndani ya ubongo au aina nyingine ya saratani ndani ya ubongo.

"Maana yake tunaweza kusema mtu yeyote anayekuja hapa BMH mwenye changamoto kama hiyo kwa ujuzi huu tulionao utatumika kumtibu, miaka yote sisi BMH tutakuwa mbele katika kufanya operesheni hizi kwa ufanisi zaidi" ameahidi Dkt. Max.

Amemalizia kwa kumshukuru Mhe Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha BMH kuwa na vifaa tiba pamoja na Watalaamu.

# Washiriki wa mafunzo ya Uangalizi Maalumu (critical care) waaswa kusambaza maarifa kwa watumishi wengine

**Washiriki** wa mafunzo ya uangalizi maalumu (critical care) wameaswa kusambaza maarifa kwa watumishi wenzao watakaporudi kwenye vituo vyao vya kazi.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) Prof. Abel Makubi, amesema mafunzo hayo yatatatua mapungufu katika huduma ya afya hasa kutoa huduma kwa wakati.

"Mafunzo haya ni muhimu wakati huu ambapo Serikali inaendelea kupanua huduma ya ICU na Matibabu ya Huduma ya Dharura," amesema Prof. Makubi

Mafunzo hayo yamewakutanisha watumishi kutoka Dodoma, Singida, Songwe, Iringa na Morogoro yaliandaliwa na Kituo cha Mafunzo ya Huduma ya Matibabu ya Magonjwa ya Dharura (EMSA) kwa kushirikiana na BMH.

Prof Makubi amefafanua kuwa mafunzo hayo yataongeza maarifa ya matibabu ya kuokoa maisha, kuwezesha viungo vya mwili vilivyopata ajali na kujeruhiwa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa EMSA, Dkt. Ramadhani Chunga, amesema tafiti zinaonyesha asilimia 56 ya wagonjwa mahututi hawapati matibabu ya msingi ya dharura hivyo asilimia 21 ya wagonjwa wanapoteza maisha ndani ya siku saba.

"Takwimu hizi zinaleta uhitaji wa kutolewa mafunzo ya msingi ya dharura ya kuokoa maisha kwa kwa vituo vyote vya afya," amesema Dkt. Chunga.

Dkt. Chunga amebainisha kuwa mpaka sasa EMSA ilitoa mafunzo kwa watoa huduma 2700 katika vituo mbalimbali vya afya nchini.

# Shirika la Tokushukai lafanya tathimini ya Mradi wa Kituo cha Upandikizaji Figo BMH

**Shirika** la Afya la Tokushukai la Tokyo, Japan limefanya tathimini ya mradi wa ujenzi jengo la huduma ya upandikizaji figo katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH).

Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Prof. Abel Makubi, ameshukuru shirika hilo kwa ushirikiano mkubwa walionao na BMH.

"Tunayo furaha kuwapokea na kuwatembeza maeneo ya Hospitali ili kufanya tathimini ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi," amesema Prof. Makubi.

Jengo hilo litakuwa maalumu kwa ajili ya vyumba vya kufanyia upasuaji na upandikizaji figo na wodi kwa ajili ya kulaza wagonjwa wa figo pamoja na watakaokuwa wamepandikizwa figo.

Prof. Makubi, ametumia fursa hiyo kutoa shukrani kwa kushirikiana kwa shirika kwa kufundisha wataalamu wa BMH mpaka kufikia kuanza upandikizaji wa figo kwa kutumia wataalamu wake

Kwa upande wake, Prof. Mwanatambwe Milanga, anayeshughulika na masuala ya mashirikiano ya Afrika katika shirika hilo, amesema shirika hilo litagharamia utekelezaji wa ujenzi wa jengo hilo.

"Nawashukuru BMH kwa ushirikiano mkubwa toka 2018 walipoanza huduma ya upandikizaji figo na sisi tukitoa msaada wa mafunzo kwa wataalamu wake," amesema Prof. Milanga.



# Mhagama Apongeza huduma za afya za BMH katika Maonesho ya Wiki ya Afya

**Waziri** wa Afya Mhe. Jenista Mhagama (MB) ameipongeza huduma za Afya zilizotolewa kwenye Banda la Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) katika Maonesho ya wiki ya Afya yaliyofanyika katika Viwanja vya ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Jijini Dodoma.

Mhe. Jenista ameyasema hayo alipotembelea banda la BMH kujionea hali ya utoaji huduma kwa wananchi wakati wa hafla ya kilele cha Maonesho ya Wiki ya Afya.

"Ni jambo la kupongezwa kuona timu ya Madaktari Bingwa wabozezi na mashine za kisasa za kufanyia vipimo na kutolea matibabu ambazo Hospitali ya Benjamin Mkapa imezileta kwenye Maonesho ya Wiki ya Afya kwa ajili ya kuhudumia wananchi. Aidha, nipongeze pia kwa namna maonesho yalivyoandaliwa na kutangazwa vizuri yameweza hadi kuwaleta wananchi wa mikoa mbalimbali kuja kutembelea maonesho na kupata huduma za matibabu" amesisitiza Mhe. Waziri Jenista.

Naye Mkuu wa Idara ya magonjwa ya mfumo wa mkojo wa BMH Dkt. Remigius Rugakingira ameeleza kuwa pamoja na vipimo vya kisasa, BMH imeleta Madaktari Bingwa katika magonjwa ya Figo, magonjwa ya Moyo, magonjwa ya Damu, elimu ya upandikizaji Uloto, magonjwa ya macho, magonjwa ya mfumo wa mkojo, magonjwa ya ndani na huduma za afya za dharura.

"tayari BMH tumehudumia wananchi zaidi ya 320 na bado idadi ya wananchi wameendelea kujitokeza kwa wingi ambayo ndio kilele" ameongeza Dkt. Remigius

Mama Magreth Kusekwa wa Ipagala Jijini Dodoma ameishukuru kwa huduma za matibabu ya macho alizozipata kwenye banda la BMH, huduma hazichelewi ndani ya muda mfupi unakuwa umekamilisha matibabu yako.

Aidha, amepongeza Wizara ya Afya kwa kuandaa maonesho ya Afya na kuzileta Taasisi nyingi za kutoa huduma za Afya chini ya mwamvuli mmoja imekuwa rahisi kwa wananchi, tunaomba maonesho haya yafanyike kila mwaka.







# BMH kuboresha kanzi data za magonjwa ili kujenga misingi bora ya huduma za tafiti




**Hospitali** ya Benjamin Mkapa (BMH) inapanga kuboresha kanzi data ya magonjwa kwa ajili ya kuboresha huduma na tafiti ili kufuatilia mwenendo wa magonjwa

Akiwasilisha Mada ya uboreshaji wa kanzi data katika CME, Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Prof. Abel Makubi, alisema uanzishaji wa kanzi data ya magonjwa ni muhimu kwa ajili ya kupata takwimu kwa kujua  na kufatilia mwenendo wa magonjwa, na kuweka misingi imara ya tafiti na ubora wa huduma.

"Tunahitaji kanzi data mbalimbali kwa ajili ya kuboresha, kumjali mgonjwa wetu na kufuatilia hali za magonjwa," amesema Prof. Makubi

Prof. Makubi amefafanua kukosekana kwa kanzi data katika Taasisi nyingi za afya imekuwa ni changamoto ya kupatikana kwa takwimu muhimu za tafiti za afya.

"Kama Taifa, tumejifunza mambo mengi kutoka Kanzi data za TB, Ukoma na HIV, lakini tumekosa mwendelezo ya kutumia rasilimanli zetu katika magonjwa mengine. Miaka michache iliyopita tulipata mlipuko wa ugonjwa wa COVID19, lakini kuna takwimu chache sana za ugonjwa huu kwa sababu ya kukosekana kanzi data endelevu kitu ambacho kinaendelea katika Magonjwa yasiyo ambukiza (NCDs) kama Moyo, kisukari na Saratani" amesema Prof. Makubi.

Mtaalamu wa utafiti BMH Dkt. Anwar Salim, alisema kanzi data itasaidia kufuatilia maendeleo ya mgonjwa na historia yake.

"Tunapoanzisha kanzi data, tunapaswa kuanzisha kamati maalumu ya kuisimamia," amesema Dkt. Salim.

Afisa TEHAMA wa BMH, Ndg. Lucas Kisinga, amesema kanzi data hii itakuwa inapatikana kwa njia kompyuta na simu janja muda wowote wataalamu wanapoihitaji.

"Tunafanyia kazi ili kanzi data ya mgonjwa iweze kupatikana kwa njia ya kompyuta na simu janja muda wowote ili kuwezesha wataalamu wanapotaka kufanya tafiti za kitaaluma," amesema Ndg. Kisinga.

Aidha wakati akichangia, Daktari Bingwa wa Mishipa ya fahamu na Ubongo, Jerome Mkiramweni, amesema uanzishaji wa kanzi data unaingiza BMH kwenye ramani ya ulimwengu.



# BMH yaondoa uvimbe wa ubongo wa ukubwa wa gram 380

**Hospitali** ya Benjamin Mkapa (BMH) imefanikiwa kunwdoa uvimbe mkubwa kwenye ubongo wa mwanamke wa umri wa miaka 32 mkazi wa Mtumba, jijini Dodoma.

Daktari Bingwa wa ubongo na mishipa ya fahamu, Dkt. Maxgama Ndosi, aliyeongoza upasuaji huo, alisema kuwa uvimbe ulikuwa upande wa kulia wa ubongo wa mgonjwa umekuwa na ukubwa wa gram 380.

“Alikuja akiwa hawezi kutembea baada ya uchunguzi wa kitabibu tukagundua ana uvimbe mkubwa kwenye ubungo ambao ulihitaji upasuaji wa haraka ili kumuokoa,” amesema Dkt. Maxgama.

Bi Olivier Udoba, ambaye ni mama mzazi wa mgonjwa huyo, aliishukuru Hospitali ya Benjamin Mkapa kwa huduma hiyo ya matibabu.

“Nawashukuru madaktari wa Benjamin Mkapa kwa huduma nzuri ya kumuokoa mwanangu,” ameongeza.

Bi Udoba alifahamisha kuwa binti yake alianza kuumwa toka mwaka jana mwezi wa Septemba na kwamba alikuwa akipata changamoto mbalimbali za kiafya ikiwemo kupata degedege.

“Mwanzoni tulikuwa tumepanga kumpeleka Dar es Salaam hivyo tulivyoona hali yake inazidi kuwa mbaya tukabadili maamuzi tukamleta hapa Hospitali ya Benjamin Mkapa,” amesema Bi Udoba.



# Dkt. Mollel aelekeza kuendelezwa kwa mafunzo ya utayari wa kudhibiti maafa

**Naibu** Waziri wa Afya, Dkt Godwin Mollel, ameelekeza kuendelezwa kwa mafunzo ya kukabiliana na maafa yaliyoratibiwa na Idara ya Magonjwa ya Dharura ya Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) na kuwezeshwa na Shirika la Maendeleo la Uturuki (TIKA).

Akiongea wakati wa hafla ya kufunga mafunzo hayo, Naibu Waziri wa Afya, Dkt Godwin Mollel, amesema ndani ya miaka minne ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amefanya mapinduzi makubwa ya maendeleo katika sekta ya afya.

"Mpaka sasa tumepokea wageni 17,000 kutoka nchi za nje ambao wamekuja kufata matibabu nchini sababu ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," amesema Dkt. Mollel.

Mafunzo hayo yaliyoratibiwa na Idara ya Magonjwa ya Dharura ya Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) na kuwezeshwa na Shirika la Maendeleo la Uturuki (TIKA) yamewaleta pamoja washiriki 32 kutoka sekta mbalimbali.

Dkt Mollel ametumia nafasi hiyo kupongeza uongozi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) na kuongeza kuwa lengo la kuipandisha Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) sasa linaenda kutimia.

"Ndani ya miaka hii miwili, lengo letu la kuipandisha Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) chini ya uongozi wa Prof Makubi, sasa linaenda kutimia na itakuwa Hospitali ya Taifa ya kipekee," ameongeza.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Prof Abel Makubi, amesema lengo la mafunzo hayo ni kuboresha mfumo wa kudhibiti maafa.


"Haya mafunzo yatasaidia timu hii kukabiliana na majanga yanapotokea. Tunamshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuboresha mifumo ya afya," Prof. Makubi.

Aidha, mwakilishi wa Wizara ya Afya wa Uturuki, Dkt. Mustapher Kucuk, amesema mpango huu unaonesha mahusiano makubwa yaliopo kati ya Tanzania na Uturuki.

"mpango huu umetuleta hapa pamoja ni uthibitisho wa ushirikiano imara tulionao kati ya Serikali ya Tanzania na Uturuki," amesema Dkt Kucuk

# Zaidi ya Sh. bilioni 28 kutumika kujenga Kituo cha Upandikizaji Figo Tanzania

## ■ Ni kikubwa katika Ukanda wa Jangwa la Sahara
## ■ Pia itatumika katika kutoa mafunzo kwa madaktari bingwa




**Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa** ameshuhudia utiaji saini wa hati ya makubaliano ya ujenzi wa kituo kikubwa cha kupandikiza figo pamoja na utoaji mafunzo kwa madaktari bingwa ambacho kitakuwa ni kikubwa katika ukanda wa Jangwa la Sahara.

Kituo hicho ambacho kitajengwa kwenye Hospitali ya Kanda ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma ni ushirikiano kati ya Shirika la Tiba la TOKUSHUKAI, Hospitali ya Benjamin Mkapa na Chuo Kikuu cha Dodoma na kinatarajia kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 28 ikiwa ni msaada usiokuwa na masharti yoyote.

Utiaji saini huo umefanyika jana (Jumatatu, Mei 26, 2025) wakati kongamano la Biashara, Uwekezaji na Utalii lililowakutanisha wafanyabiashara wa Tanzania na wafanyabiashara na wawekezaji wa Japan katika ukumbi wa mikutano wa Hoteli ya Westin, Osaka, Japan, ikiwa ni sehemu ya ushiriki wa Tanzania katika maonersho ya World Expo Osaka 2025. Kongamano hilo

# Sh. bilioni 28 kujenga Kituo cha Upandikizaji Figo




lilifunguliwa na Mheshimiwa Majaliwa.

Akizungumza baada ya utiaji saini huo Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamini Mkapa, Profesa Abel Makubi amesema wamesaini makubaliano na shirika hilo linaloundwa na kundi la madaktari Wakijapan ambao wamekuwa wakisaidia utoaji na uboreshaji huduma za afya. "Hawa ni wadau wetu wa muda mrefu na walikuwa watu wa kwanza kusaidia utoaji wa huduma Dialysis katika hospitali ya Benjamin Mkapa."

"MOU hii ambayo tumeisaini sasa hivi ni kwa ajili ya kujenga kituo cha umahiri katika upandikizaji figo kwenye eneo la Tanzania na Ukanda wa Jangwa la Sahara."

Amesema mbali na ujenzi wa kituo hicho ambacho kitajengwa ndani ya hospitali ya Benjamin Mkapa na kutarajiwa kukamilika na kuanza kutoa huduma ndani ya miaka mitatu, pia Serikali ya Tanzania imejipanga kusaidia baadhi ya maeneo ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati. Ujenzi wa kituo hicho unarajiwa kuanza mwaka huu.

"Tunatoa shukurani kwa Serikali ya Japan kupitia wadau hao na tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira wezeshi ambayo yametufanya sisi tuweze kufikia makubaliano na wadau hawa. Makubaliano haya yanakwenda kusaidia wananchi kwa ajili ya kuboresha huduma za figo si kwa Watanzania tu bali kwa Waafrika wengine."

Profesa Makubi amesema pia kituo

# Sh. bilioni 28 kujenga Kituo cha Upandikizaji Figo




hicho kitakuwa kinatoa mafunzo kwa ajili ya kupandikiza figo, pamoja na kufanya tafiti kwa ajili ya kuzuia au kupunguza magonjwa yanayohusiana na figo. Mafunzo yatolewa kwa ushirikiano kati ya Hospitali ya Benjamin Mkapa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Profesa Lugano Kusiluka amesema makubaliano hayo yataimarisha huduma ya upandikizaji figo ambao unafanyika katika Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma kwa ushirikiano wa wataalamu wa hospitali hiyo pamoja na wa UDOM.

Amesema kwa sasa UDOM ipo katika mchakato wa kuanzisha programu ya uhandisi wa vifaa tiba ili kuounguza gharama kwa Serikali kutumia wataalam kutoka nje ya nchi kutengeneza vifaa hivyo mara vinapoharibika. "Kwa makubaliano haya mbali na kufundisha wataamu kutengeneza vifaa hivyo, pia watafundisha namna ya kuvitunza ili visiharibike."

Pia, Profesa Kusiluka amesema katika makubaliano hayo Tanzania inakwenda kunufaika kwa kuwa kituo kikubwa cha upandikizaji figo inachotarajiwa kujengwa kitatumika katika kufundisha madaktari bingwa pamoja na wataalam kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika kupandikiza figo na baadae kupandikiza viungo vingine.

Hati nyingine iliyosainiwa ni kati ya ushirikiano kati Chuo Kikuu cha Dodoma na Hospitali ya Benjamin Mkapa na Chama cha Maendeleo na Uchumi Afrika cha Japan (AFRECO), hati hizo ni sehemu ya hati sita za makubaliano zilizosainiwa leo kati ya Serikali Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na mashirika ya Japan.

# Mabalozi wakagua ubora wa huduma zitolewazo BMH





**Mabalozi** wanaowakilisha nchi mbalimbali hapa nchini Tanzania wametembelea Hospitali ya Benjamin Mkapa kujionea huduma zinazotolewa.

Mabalozi hao walioongozwa na Waziri wa Mambo ya nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Mahmoud Thabit Kombo pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mh. Rosemary Senyamule, kuitembelea Hospitali wamejionea huduma mbalimbali ikiwemo Idara ya Magonjwa ya Dharura na wodi maalumu za viongozi.

Kwaupande wake Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Dkt. Kessy Shija amesema BMH ipo na wataalam wa viwango vya juu na inatoa huduma za matibabu ya kibingwa na bingwa bobezi na ipo tayari kuwa hudumia mabolozi watakapo hamia hapa Dodoma.

"BMH ina wataalam waliobobea katika maeneo mbalimbali, wataam waliobobea katika magonjwa ya dharua, figo, moyo, ubongo, upasuaji wa matundu madogo, wanawake, njia ya mkojo, watoto na magonjwa mengine mbalimbali, tupo tayari kuwahudumia kwa viwango vya juu kabisa", amesema Dkt. Shija.

Dkt. Shija ameongeza kwa kuwashukuru Waziri Mahmoud Thabit Kombo na Mkuu wa Mkoa Mhe. Rosemary Senyamule kwa kuongoza ziara hiyo ya mabalozi kutembelea BMH.

"Namshukuru Mhe. Waziri Kombo na Mkuu wa Mkoa Senyamule kwa kuongoza ziara ya mabalozi kuweza kuitangaza Dodoma kupitia hospitali yetu ya Benjamin Mkapa kujionea huduma za ubingwa wa juu zinazotolewa " amesema Dkt. Shija.

**Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano Hospitali ya Benjamin Mkapa**

